Biblia inasema katika kitabu cha Mwanzo.

> *Mwanzo 4:1 Adamu akamjua Hawa mkewe; naye akapata mimba, akamzaa Kaini, akasema, Nimepata mtoto mwanamume kwa Bwana.*
>
> *2 Akaongeza akamzaa ndugu yake, Habili. Habili alikuwa mchunga kondoo, na Kaini alikuwa mkulima ardhi"*

Mtoto mwingine aliyezaliwa na Adamu na Hawa alikuwa ni Sethi.

> *Mwanzo 5:1 "Hiki ndicho kitabu cha vizazi vya Adamu. Siku ile Mungu alipoumba mtu, kwa sura ya Mungu alimfanya;*
>
> *2 mwanamume na mwanamke aliwaumba, akawabariki akawaita jina lao Adamu, siku ile walipoumbwa.*
>
> *3 Adamu akaishi miaka mia na thelathini, akazaa mwana kwa sura yake, kwa mfano wake, akamwita jina lake Sethi"*

Lakini pia Biblia haiishi hapo, inasema Adamu alizaa watoto wengine wakiume na wakike baada ya kumzaa Sethi.

> *Mwanzo 5:4 “Siku za Adamu baada ya kumzaa Sethi zilikuwa miaka mia nane, akazaa wana, waume na wake”.*

Na hao watoto wakike waliozaliwa ndio waliokuja kuwa wake wa hao watoto wengine wa kiume wa Adamu.

Hivyo Biblia  haitoi idadi kamili ya watoto wa Adamu, pengine walikuwa 5 au 10 au 20 au 30, hatujui lakini zaidi ya Sethi, walikuwapo pia watoto wengine wa Adamu ambao habari zao hazikuandikwa katika biblia.

ADAMU ALIISHI MIAKA MINGAPI?

Jibu tunalipata katika Mstari wa 5

> *Mwanzo 5:5 “Siku zote za Adamu alizoishi ni miaka mia kenda na thelathini, naye akafa.”*

Kwahiyo siku zote za Adamu ilikuwa ni miaka 980, akafa

---

Mada Nyinginezo:

JE! ADAMU ALIWASALIANA NA MUNGU KWA LUGHA IPI PALE BUSTANINI?

UZAO WA NYOKA NI UPI?.

MTI WA UZIMA NA MTI WA MAARIFA NI UPI?.

---

Rudi Nyumbani:

Share on:
WhatsApp